RPS RICHMOND PUBLIC SCHOOLS

# Sheria za Haki za Mwanafunzi, Mzazi na Mtunzaji

Watoto wote wana haki ya kupata elimu ya bila malipo. Wanafunzi wote wanapaswa kuwa na kila fursa inayowezekana ili kutimiza ndoto zao, kwa hivyo ni muhimu kwamba familia zijue haki zao za kisheria ili kuhakikisha upatikanaji na ushiriki wenye usawa katika mfumo wetu wa elimu.

**Wanafunzi wana haki ya kutendewa kwa usawa na wana haki ya kuwa salama katika shule zao za umma.**

- Shule haziruhusiwi kuwabagua wanafunzi kwa misingi ya mbari, dini, rangi, asili ya utaifa, mapenzi[1], mwelekeo wa jinsia, jinsia, utambulisho wa kijinsia, ulemavu, kabila, ukoo, hali ya ndoa au ya mzazi au kwa misingi yoyote iliyopigwa marufuku na sheria.
- Shule lazima zilinde wanafunzi dhidi ya unyanyasaji na uchokozi.[2]
- Shule hazipaswi kuwazuia wanafunzi wajawazito au wanafunzi wenye watoto kwenda shuleni. Shule lazima zitoe hali za ziada ili wanafunzi hao waweze kukamilisha kazi za darasani, na kuwaruhusu kushiriki katika shughuli za nje ya masomo.[3]

**Wanafunzi wana uhuru wa dini, kusema na wa kujieleza.**

- Almradi itikadi za imani yao hazivurugi elimu ya wanafunzi wengine kwa kiasi kikubwa, wanafunzi wote wanaweza:
  - kueleza maoni na imani zao shuleni;[4]
  - kusali peke yao shuleni;;[5]
  - Kuja na vitabu vya kidini shuleni;
  - kuvaa mavazi ambayo ni sehemu ya imani yao ya kidini (mifano ni pamoja na hijabu, yarmulke, au msalaba wa sanamu) au mtindo wa nywele ambao kwa kawaida unachukuliwa kuwa sehemu ya urithi wa kikabila wa mtu huyo;[6]
  - kuzungumza kuhusu imani yao shuleni na katika kazi za mwanafunzi;[7]
  - kuunda vilabu au mashirika ya kidini ambayo hukutana kabla au baada ya shule; [8] na
  - kuruhusiwa kutohudhuria shule kwa ajili ya kuadhimisha sikukuu za kidini.[9]
- Shule za umma hazipaswi kuegemea upande wowote kuhusiana na dini, wala kusaidia au kupinga dini.[10]
- Sala zilizopangwa za shuleni au ujielezaji mwingine wa kidini unaoongozwa na wafanyakazi wa kitengo cha shule hauruhusiwi. Wanafunzi na wafanyakazi wanaweza kushiriki katika nyakati za ukimya.[11]
- Wanafunzi wana haki ya kuunda vilabu shuleni vinavyoonyesha utambulisho au imani zao, ikiwa ni pamoja na utambulisho wa kitamaduni na kijinsia.
- Shule lazima zitoe ufikiaji sawa wa fursa za shuleni, ikiwa ni pamoja na uundaji wa vilabu.

**Wanafunzi na familia wana haki ya kujiondoa kwenye masharti na shughuli zinazokinzana na imani zao, kama inavyoruhusiwa na sheria ya eneo, jimbo na shirikisho. Wazazi wana haki ya kuchagua mtoto wao asishiriki katika:**

- Elimu ya maisha ya familia.[12]
- Baadhi ya chanjo.[13]

- Elimu ya shule za umma. Wazazi wanaweza kuchagua kuwasomesha watoto wao nyumbani au kuwapeleka katika shule ya kibinafsi au ya kujitegemea. Hata hivyo, watoto wote lazima wapokee aina fulani ya elimu kulingana na sheria za mahudhurio ya lazima.[14]

**Wanafunzi na familia zinazozungumza lugha nyingine isipokuwa Kiingereza zina haki ya kupata fursa sawa na wazungumzaji wa Kiingereza.**

- Wanafunzi wa Kiingereza (EL) wana haki ya kupata fursa sawa ya kushiriki katika mipango yote ya kimasomo na ya nje ya masomo inayolingana na umri.[15]
- Wanafunzi wote wa EL wana haki ya kufundishwa kwa lugha ya Kiingereza.[16] Wazazi wanaweza kuchagua kuwaondoa watoto wao kwenye mipango ya EL au huduma fulani.
- Ukosefu wa ufasaha wa Kiingereza hauwezi kutumiwa kumweka mwanafunzi kwenye huduma za elimu ya kipekee. Wanafunzi wa EL wenye ulemavu wa kimasomo lazima wapewe huduma za mafundisho ya lugha na huduma zinazohusiana na ulemavu.[17]
- Watoto ambao hawajaandikishwa rasmi nchini wana haki ya kupata elimu ya shule za umma.[18] Rekodi ya kuzaliwa au ithibati nyingine ya kuaminika ya utambulisho na umri wa mwanafunzi inahitajika ili kusajiliwa.[19] Shule hazipaswi kuwauliza wazazi au wanafunzi kuhusu hali yao ya uhamiaji. Huenda shule zisihitaji wanafunzi au wazazi watoe nambari ya ustawi ya jamii.[20]
- Wazazi wa wanafunizi wa EL wana haki ya kupokea mawasiliano katika lugha wanayoweza kuelewa kupitia huduma za tafsiri na ukalimani, na kupokea taarifa kuhusu mpango, huduma au shughuli yoyote ya shule.[21]

**Wanafunzi waliotambuliwa kuwa na ulemavu wana haki ya kupata fursa sawa na wenzao wasio na ulemavu.**

- Ikiwa mtoto anashukiwa kuwa na ulemavu, wazazi na walezi wana haki ya kuomba mtoto wao atathminiwe kama ana ulemavu. [22]Iwapo mwanafunzi atapatikana kuwa na ulemavu, lazima apewe:
    - Mpango wa elimu binafsi[23], au mpango wa kifungu cha 504[24], unaojumuisha huduma, na/au marekebisho ambayo humruhusu mwanafunzi kutumia mtaala wa elimu ya jumla na/au kufanya maendeleo muhimu ya kielimu katika mtaala wa elimu ya jumla;
    - Ufikiaji sawa wa madarasa ya kimasomo, safari za nje, shughuli za nje ya masomo, teknolojia ya shule na huduma za afya.
    - Mafundisho katika mazingira yenye vikwazo vichache zaidi.[25]
- Wazazi wanaweza kualika watu ambao wana ujuzi kuhusu mtoto au mahitaji yake ya kielimu kuhudhuria mikutano ya IEP.[26]
- Wanafunzi walio na mipango ya IEP au mipango ya Kifungu cha 504 ambao wamesimamishwa shule kwa zaidi ya siku 10 au waliofukuzwa lazima wapewe aina mbadala ya elimu.[27]
- Ikiwa mzazi au mwanafunzi hakubaliani na uamuzi wa timu ya IEP, ana haki ya kukata rufaa.
    - Anaweza kuomba mkutano mwingine wa timu ya IEP kabla ya kuanza mchakato wa kukata rufaa.
        - Wasiwasi kuhusu huduma za elimu maalum unapaswa kutumwa kwa njia ya maandishi kwa shule. Wazazi au walezi wanapaswa kuhifadhi nakala ya hati zote.
    - Ikiwa mzazi au mlezi wa kisheria hakubaliani na uamuzi wa timu ya IEP, ana haki ya kuwasilisha malalamiko kwa Idara ya Elimu ya Virginia.

- Kwa maelezo zaidi kuhusu kusuluhisha migogoro, kuwasilisha malalamiko, na kuwasilisha maombi ya usikilizwaji kwa mchakato wa haki, tembelea tovuti ya Idara ya Elimu ya Virginia katika https://www.doe.virginia.gov/special_ed/resolving_disputes.

**Wanafunzi wanaokabiliwa na ukosefu wa makazi wana haki ya:**

- Kubaki katika shule yao ya sasa au ya hivi majuzi kwa muda uliosalia wa shule au kujiandikisha katika shule ya eneo wanaloishi.[28]
- Kupata huduma za usafiri wa kwenda na kurudi shuleni, hata kama wanahamia nje ya jiji.[29]

**Wanafunzi, wazazi na walezi wana haki ya:**

- Kupokea nakala za rekodi za kimasomo na nidhamu. Vitengo vya shule vina hadi siku 45 kutii ombi la kufikia rekodi.[30]
- Kupokea taarifa zilizoandikwa za kufukuzwa au kusimamishwa shule.[31]
- Kukata rufaa kwa maamuzi yoyote ya kinidhamu yaliyotolewa na msimamizi wa shule, afisa wa usikilizaji, au Kamati ya Nidhamu ya Bodi ya Shule (ikiwa si uamuzi wa pamoja wa Kamati).[32]

## Dondoo

---

[1] 20 U.S.C.A. §1681
[2] Va. Code §22.1-276.01 ; 22.1-279.6
[3] 34 C.F.R. §106.40
[4] Tinker v. Des Moines Independent School District, 393 U.S. 503, 89 S.Ct. 733
[5] 20 U.S.C.§7904, *Santa Fe Independent School Dist. v. Doe*, 530 U.S. 290, 313, 120 S.Ct. 2266, 2281 (2000)
[6] Va. Code §22.1-279(I)
[7] Va. Code §22.1-203.3
[8] *Board of Educ. of Westside Community Schools v. Mergens By and Through Mergens*, 496 U.S. 226, 110 S.Ct 2356 (1990)
[9] Va. Code §22.1-254
[10] 374 U.S. 203, 225, 83 S.Ct. 1560, 1573 (1963)
[11] *Santa Fe Independent School Dist. v. Doe*, 530 U.S. 290, 120 S.Ct. 2266; Va. Code§ 22.1-203.1
[12] Va. Code §22.1-207.2
[13] Va. Code §32.1-46
[14] Va. Code §22.1-254 §22.1-254.1
[15] *Plyler v. Doe*, 457 U.S. 202, 102. S.Ct. 2382 (1982)
[16] VA. Code §22.1-212.1
[17] 20 U.S.C.A. §1703
[18] *Plyler v. Doe*, 457 U.S. 202, 102. S.Ct. 2382 (1982)
[19] Va. Code §22.1-3.1 Sheria hii inatumika kwa wanafunzi wote, bila kujali kama walizaliwa Marekani au wamehamia Marekani.
[20] Va. Code §22-287.03. Sheria hii inatumika kwa wanafunzi wote, bila kujali kama walizaliwa Marekani au wamehamia Marekani.
[21] 20 U.S.C.A. §1703

[22] 8 VAC 20-81-50
[23] 8 VAC 20-81-110
[24] Kifungu cha 504 cha Sheria ya Urekebishaji ya 1973
[25] 8 VAC 20-81-130
[26] 8 VAC 20-81-110
[27] 8 VAC 20-81-160
[28] McKinney Vento Act, 42 U.S.C. §11432(g)(3)(A)
[29] McKinney Vento Act, 42 U.S.C. 11432(g)(1)(J)(iii))
[30] Family Educational Rights and Privacy Act ("FERPA"), 20 U.S.C. § 1232(g); Va. Code 22.1-287(A).
[31] Va. Code §22.-277.04, §22.-277.05, §22.-277.06
[32] Va. Code §22.-277.04, §22.-277.05, §22.-277.06